

HERITAGE DRINKING WATER LIMITED



NAFASI ZA KAZI ZA MGAHAWA

KAMPUNI ya Heritage Drinking Water Limited ilianzishwa April 7, 2020. Nje ya kuchakata na kuuza maji, kampuni imefungua Mgahawa Mzuri Sana, mkoani Mwanza, katika mji wa Kisesa. Ili kuleta ufanishi, Kampuni inatangaza nafasi 20 za wahudumu (service), nafasi 5 za wapishi, nafasi 3 za wasimamizi au meneja, nafasi 3 za madereva wa pikipiki na gari (vyote), na nafasi 2 za walini za usiku na mchana kwa ajili ya kuendesha vizuri Mgahawa wake uitwao HERITAGE DELICIOS FOOD uliopo stendi ya pili ya Magu. Kama una sifa za mwombaji tafadhalii tuma faili moja la PDF la maombi yako YOTE kwenye namba hii +255 742 000 678 kwa njia ya WhatsApp tu.

SIFA ZA MWOMBALI

- Awe anajitambua na kujielewa
- Awe mwaminifu, asiwe ana tabia ya wizi au udokozi
- Awe mchangamfu na mwenye tabasamu kwa wateja anaowahudumia
- Awe shapu sana kuhudumia wateja wengi na bila kupata hasara
- Awe na lugha nzuri kwa wateja na mvumilivu kwa yatokanayo na wateja
- Awe mwaminifu, awe na hofu ya Mungu
- Awe na uwezo wa kuhudumia wateja akiwa amesimama kwa mda wote wa kazi
- Awe mwenyeji au mkazi wa Mwanza wakati wa kazi hii
- Awe amesomea hotelia, huduma kwa wateja au utawala chuo kinachotambulika
- Elimu: fomu 4, au cheti, au fomu 6, au shahada yoyote ya Tanzania
- Awe tayari kupokea mafunzo ya kazi na kujitelea kwa wiki moja

Mwisho wa kutuma maombi: **8 Machi 2024** saa 10 jioni kamili.

Viambatanisho vya maombi vifuatavyo vitumwe kama PDF faili moja kwenda +255 742 000 678 kwa njia ya WhatsApp tu:

1. Wasifu/ CV;
2. Barua ya maombi ya mkuu (siyo kompyuta);
3. Barua ya mtendaji wa mtaa AU kopi ya kitambulisho cha NIDA;
4. Barua ya mdhamini yenye picha yake, NIDA, na simu yake;
5. Pasipoti saizi (picha) mbili; na,
6. Kielelezo kuwa ana simu janja/ smartphone (kwa ajili ya kutuma ripoti).

Anuanzi:

P.O. BOX 55150, Dar Es Salaam, Tanzania. Changanyikeni, Shina No. 5, Block 40.

Simu ya kampuni kwa manlizo na jinsi ya kufika Kisesa: +255 656 000 678 (usipige +255742000678 tafadhalii sana)

Usaili: 9 au 10 Machi 2024, Kuanza kazi: 18 Machi 2024.